yako. Pia, una haki ya kukataa kuchakatwa au kuhamishwa kwa maelezo yako kwenye huduma nyingine.

Iwapo una maswali au maombi zaidi yanayohusiana na haki zako, unaweza kuwasiliana na Google na afisa wetu wa ulinzi wa data. Unaweza pia kuwasiliana na mamlaka ya ulinzi wa data ya eneo uliko ikiwa una matatizo kuhusu haki zako kwa mujibu wa sheria za eneo uliko.

## Kidhibiti cha data

Isipokuwa ibainishwe vinginevyo katika ilani ya faragha ya huduma mahususi, wadhibiti wa data walio na wajibu wa kuchakata taarifa zako hutegemea mahali uliko:

- Google Ireland Limited kwa watumiaji wa huduma za Google walio kwenye nchi washirika katika Makubaliano ya Kiuchumi ya Ulaya au Uswizi, inapatikana katika Gordon House, Barrow Street, Dublin 4, Ayalandi.
- Google LLC kwa watumiaji wa huduma za Google walio Uingereza, inapatikana 1600 Amphitheatre Parkway, Mountain View, California 94043, Marekani.

Google LLC ndiye mdhibiti wa data aliye na wajibu wa kuchakata maelezo yaliyoainishwa na kuonyeshwa katika huduma kama vile Tafuta na Google na Ramani za Google bila kujali eneo uliko. Google Ireland Limited ndiye mdhibiti wa data aliye na wajibu wa kuchakata maelezo ya kuipa mafunzo miundo ya AI ya Google kwa madhumuni ya kuitumia katika huduma zinazotolewa na Google Ireland Limited kwenye nchi washirika katika Makubaliano ya Kiuchumi ya Ulaya au Uswizi.

## Misingi ya kisheria ya uchakataji

Tunachakata maelezo yako kwa madhumuni yaliyoelezwa katika sera hii, kulingana na misingi ifuatayo ya kisheria:

- Tunachakata data yako ili kukupa huduma uliyoomba kwa mujibu wa mkataba.
- Tunachakata data yako kwa sababu zetu halali na zile za wengine huku tukitekeleza ulinzi stahiki kwa ajili ya faragha yako.
- Tunachakata data yako inapohitajika ili kulinda maslahi yako muhimu au ya mtu mwingine.

- Tunachakata data yako wakati tuna wajibu wa kisheria kufanya hivyo.
- Tunaomba idhini yako ili kuchakata data yako kwa madhumuni mahususi na una haki ya kuondoa idhini yako wakati wowote.

Jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako ya faragha itabaini aina ya data itakayochakatwa, madhumuni ya kuchakata data hii na misingi ya kisheria ya kuchakata data. Jedwali lililo hapa chini linafafanua madhumuni haya ya uchakataji, aina za data inayochakatwa na misingi ya kisheria ya kuchakata data hii, kwa kina zaidi.

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| **Ili kutoa vipengele, bidhaa na huduma za Google**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Tunachakata hoja unazotafuta ili kuonyesha matokeo.<br>• Tunatumia anwani ya IP ya kifaa chako ili kukutumia data uliyoomba, kama vile kupakia video ya YouTube.<br>• Tunatumia vitambulishi mahususi vilivyohifadhiwa katika vidakuzi kwenye kifaa chako ili kutusaidia kukuthibitisha kuwa mtu anayepaswa kufikia Akaunti yako ya Google.<br>• Picha na video unazopakia katika programu ya Picha | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  • Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi. | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Ili **kutekeleza mkataba** nawe, kama vile kupakia video ya YouTube, au kuchakata, kutimiza au kufikisha oda yako unaponunua huduma au bidhaa halisi kutoka kwetu.<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  • **Kutoa, kudumisha na kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wetu**. Kwa mfano, kutumia maelezo ya |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| kwenye Google hutumiwa kukusaidia kubuni albamu, kolagi na kazi nyingine unazoweza kushiriki.<br>• Unaponunua huduma au bidhaa halisi kutoka kwetu, tunatumia anwani ya mahali bidhaa zako zitapelekwa au maagizo ya usafirishaji kwa ajili ya mambo kama vile kuchakata, kutekeleza na kusafirisha oda yako na kukupa usaidizi unaohusiana na bidhaa au huduma unayonunua.<br>• Tunachakata maelezo yako ya malipo unaponunua nafasi ya ziada ya hifadhi katika Hifadhi ya Google.<br>• Tunaweza kutumia maelezo ya mawasiliano (kama vile majina na anwani za barua pepe) ya watu unaowasiliana nao katika bidhaa za Google ili kufanya iwe rahisi kupata unayemtafuta wakati unataka kushiriki na kuwasiliana na watu hawa katika huduma | • Taarifa binafsi unazotupa unapofungua Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu:<br>• Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za | mawasiliano (kama vile majina na anwani za barua pepe) ya watu unaowasiliana nao katika bidhaa za Google ili kufanya iwe rahisi zaidi kupata unayemtafuta wakati unataka kushiriki na kuwasiliana na watu hawa katika huduma nyingine za Google, kama vile Gmail, Picha na Mratibu.<br>• Kupitia **idhini** yako, kama vile unapochagua kushiriki mahali ulipo kupitia Kipengele cha Google cha Kushiriki Mahali Ulipo. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| waweze kukupata kwenye ramani, au wajue muda wako wa makadirio wa kuwasili.<br>• Jinsi ilivyofafanuliwa katika sehemu ya Kushiriki taarifa zako, tutashiriki taarifa binafsi nje ya Google ukituruhusu. Na tutakupa vidhibiti vya kukagua na kudhibiti tovuti na programu za wengine ambazo umezipa uwezo wa kufikia data katika Akaunti yako ya Google. | Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambulizi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma. | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| | • Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |
| **Ili kudumisha na kuboresha vipengele, bidhaa na huduma za Google**<br><br>**Kudumisha huduma ili ifanye kazi ipasavyo, kama vile utatuzi wa hitilafu za huduma, kufuatilia matatizo au kutatua matatizo.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br><br>• Tunaendelea kufuatilia mifumo yetu ili kubaini matatizo. Na tukipata hitilafu katika kipengele mahususi, ukaguzi | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br><br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  • Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br><br>• Ili **kutekeleza mkataba** nawe, kama vile kutumia kumbukumbu za mitagusano yako na programu za Google ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi ipasavyo.<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo: |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| wa maelezo ya shughuli yaliyokusanywa kabla ya tatizo kuanza huturuhusu kutatua matatizo haraka zaidi.<br>• Tunaweka kumbukumbu ya mitagusano ya watumiaji na vitufe kwenye programu kama vile Ramani za Google na Tafuta ili kutusaidia kufahamu iwapo vinafanya kazi ipasavyo.<br><br>**Ili kuboresha huduma za Google na kusaidia kuboresha usalama na uaminifu wa huduma hizi, kama vile kutambua, kuzuia na kushughulikia ulaghai, matumizi mabaya, hatari za usalama na matatizo ya kiufundi ambayo yanaweza kuathiri huduma au watumiaji.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Tunachanganua data kuhusu mitagusano yako na huduma zetu ili kutusaidia kubuni bidhaa bora. Kwa mfano, inaweza kutusaidia kugundua kuwa inawachukua watu muda mwingi | malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi.<br>• Taarifa binafsi unazotupa unapofungua Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu:<br>• Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo | • **Kutoa, kudumisha na kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wetu.** Kwa mfano, kuchanganua hoja za utafutaji ambazo huandikwa vibaya mara nyingi, ili kutusaidia kuboresha vipengele vya kukagua tahajia vinavyotumiwa kwenye huduma zetu.<br>• **Kufahamu jinsi watu hutumia huduma zetu ili kuhakikisha na kuboresha utendaji wa huduma zetu.** Kwa mfano, kuchanganua matumizi ya Google Tafsiri ili kuboresha ubora wa tafsiri na kuongeza upatikanaji wa huduma ya Tafsiri katika lugha nyingi.<br>• **Kufanya utafiti unaoboresha** |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| kukamilisha jukumu fulani au wanatatizika kukamilisha hatua kwa jumla. Kisha tunaweza kubuni upya kipengele hicho na kuboresha bidhaa kwa manufaa ya kila mtu.<br>• Tunachanganua hoja za utafutaji ambazo huandikwa vibaya mara nyingi ili kutusaidia kuboresha vipengele vya kikagua tahajia, vinavyotumiwa kwenye huduma zetu.<br>• Tunachanganua matumizi ya Google Tafsiri ili kuimarisha ubora wa tafsiri na kuongeza upatikanaji wa huduma ya Tafsiri katika lugha nyingi.<br>• Tunachanganua hoja kwenye Google Shopping ili kubaini aina za bidhaa, wauzaji na chapa zinazofaa aina tofauti za hoja.<br>• Kipengele cha Kuvinjari Salama kwenye Google Chrome kinaweza kutuma maelezo kuhusu tovuti za kutiliwa shaka kati ya | kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za kuacha kufanya kazi na shughuli za mfumo).<br>• Maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile hoja zako za utafutaji, historia ya kuvinjari kwenye Chrome ambayo umesawazisha na Akaunti yako ya Google, mara unazotazama na kutumia maudhui na matangazo na shughuli zako kwenye tovuti na programu za wengine zinazotumia huduma zetu. Unaweza | **huduma zetu kwa watumiaji wetu na kunufaisha umma.** Kwa mfano, kuboresha ubora wa tafsiri katika Google Tafsiri na kuongeza upatikanaji wa huduma ya Tafsiri katika lugha nyingi. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| kivinjari cha mtumiaji na seva za Google ili kusaidia kulinda dhidi ya wizi wa data binafsi, programu hasidi, matangazo hasidi na zaidi. | kukagua na kudhibiti data ya shughuli inayohifadhiwa kwenye Akaunti yako ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |
| **Kusanidi matoleo mapya ya vipengele, bidhaa na huduma za Google**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Kufahamu jinsi watu walivyopanga picha zao katika Picasa, programu ya kwanza ya picha katika Google, kulitusaidia kubuni na kuzindua | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Mambo unayobuni au kutupa: | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  • **Kubuni bidhaa na vipengele** |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| programu ya Picha kwenye Google.<br>• Kufahamu jinsi watumiaji wanavyoangalia na jinsi watayarishi wanavyobuni maudhui mafupi kulisaidia Google kubuni huduma mpya za YouTube.<br>• Kulingana na mipangilio yako, tunaweza kuhifadhi rekodi za sauti za mitagusano ya sauti na huduma kama vile Tafuta na Google, Mratibu, Ramani na Gboard, ili kubuni na kuboresha teknolojia za sauti katika Google.<br>• Tunatumia maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao au vyanzo vingine vya umma ili kusaidia kufunza miundo mipya ya mashine kujifunza na kubuni teknolojia za msingi zinazowezesha bidhaa mbalimbali za Google kama vile Google Tafsiri, Programu za Gemini na uwezo wa AI ya Wingu. | • Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi.<br>• Taarifa binafsi unazotupa unapofungua Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu:<br>• Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi | **vipya ambavyo ni muhimu kwa watumiaji wetu.** Kwa mfano, kufahamu jinsi watu walivyotumia picha katika Picasa, programu ya kwanza ya picha katika Google, kulitusaidia kubuni na kuzindua programu ya Picha kwenye Google. Au kutumia maelezo ambayo yanapatikana hadharani kwenye mtandao au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma ili kusaidia kufunza miundo ya AI ya Google na kubuni bidhaa na vipengele kwa kutumia teknolojia hizi za msingi, kama vile Google Tafsiri, Programu za Gemini na uwezo wa AI ya Wingu.<br>• **Kutoa, kudumisha na kuboresha huduma ili** |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| • Tunatumia mitagusano yako na miundo ya AI na teknolojia kama vile Programu za Gemini ili kubuni, kufunza, kurekebisha na kuboresha miundo hii ili kushughulikia vyema maombi yako na kusasisha viainishi na vichujio vyake kwa ajili ya usalama, ufahamu wa lugha, ukweli na zaidi. | mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za kuacha kufanya kazi na shughuli za mfumo).<br>• Maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile hoja zako za utafutaji, historia ya kuvinjari kwenye Chrome ambayo umesawazisha na Akaunti yako ya Google, mara unazotazama na kutumia maudhui na matangazo | **kukidhi mahitaji ya watumiaji wetu.** Kwa mfano, kutumia maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile mitagusano yako na Programu za Gemini, ili kufunza na kuboresha miundo ya mashine kujifunza na kusasisha uwezo wake wa kuelewa lugha, vichujio na vianishi vya usalama.<br>• Kupitia **idhini** yako, kama vile kuhifadhi rekodi za sauti za mitagusano ya sauti na huduma za Tafuta na Google, Mratibu, Ramani na Gboard, ili kubuni na kuboresha teknolojia za sauti katika Google. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | na shughuli zako kwenye tovuti na programu za wengine zinazotumia huduma zetu. Unaweza kukagua na kudhibiti data ya shughuli inayohifadhiwa kwenye Akaunti yako ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |
| **Kutoa huduma zilizowekewa mapendeleo, ikiwa ni pamoja na maudhui na matangazo** | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| **Ili kuweka mapendeleo kwenye huduma zetu kwa ajili yako, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo, maudhui yaliyowekewa mapendeleo na matokeo ya utafutaji yaliyowekewa mapendeleo.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Kipengele cha Google cha Ukaguzi wa Usalama kina vidokezo vya usalama vinavyotokana na jinsi unavyotumia bidhaa za Google.<br>• Google News inaweza kukupa matokeo ya habari za karibu nawe kulingana na eneo linalokadiriwa.<br>• Huduma ya Tafuta na Google inaweza kukupa matokeo kulingana na eneo linalokadiriwa.<br>• Huduma ya Mratibu wa Google inaweza kutumia anwani zako kutuma ujumbe ukiomba, kama vile “Tuma ujumbe kwa John Smith.” | lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  ◦ Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi.<br>  ◦ Taarifa binafsi unazotupa unapofungua Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu: | yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Ili **kutekeleza mkataba** nawe, kama vile wakati huduma ya Mratibu wa Google inatumia anwani zako kutuma ujumbe unapoomba, kama vile “Tuma ujumbe kwa John Smith.”<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  ◦ **Kuweka mapendeleo kwenye huduma zetu ili kukupa hali bora ya utumiaji.** Kwa mfano, kuonyesha Google Doodle kwenye ukurasa wa kwanza wa huduma ya Tafuta ili kusherehekea tukio mahususi katika nchi uliko, kutoa vidokezo vya usalama vinavyotokana na jinsi unavyotumia bidhaa za Google, au kufanya hali ya utumiaji |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| • Programu ya Google Play hutumia maelezo kama vile programu ambazo tayari umesakinisha na video ambazo umetazama kwenye YouTube, ili kupendekeza programu mpya ambazo unaweza kupenda.<br>• Tunaweza kuonyesha Google Doodle kwenye ukurasa wa kwanza wa huduma ya Tafuta ili kusherehekea tukio mahususi katika nchi uliko.<br>• Google inaweza kukuonyesha matangazo kulingana na muktadha wa tovuti unayotembelea, kama vile matangazo ya vifaa vya bustani kwenye ukurasa unaohusu vidokezo vya kilimo cha bustani.<br>• Wakati umeingia katika Akaunti yako ya Google na umewasha kidhibiti cha Historia ya Shughuli kwenye Wavuti na Programu, unaweza kupata | • Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za kuacha kufanya kazi na shughuli za mfumo).<br>• Maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile hoja zako za utafutaji, historia ya kuvinjari kwenye Chrome ambayo umesawazish | iambatane na umri panapofaa.<br>• **Kutoa utangazaji, hali inayoturuhusu kutoa huduma zetu nyingi bila malipo.** Kwa mfano, kukuonyesha matangazo kulingana na muktadha wa tovuti unayotembelea, kama vile matangazo ya vifaa vya kilimo cha bustani kwenye ukurasa kuhusu vidokezo vya kilimo cha bustani. (Na wakati matangazo yamewekewa mapendeleo, tunaomba idhini yako.)<br>• Kupitia **idhini** yako, kama vile kupendekeza programu kwenye Google Play kulingana na video ulizotazama kwenye YouTube, au kukuonyesha matangazo yaliyowekewa mapendeleo kulingana na mambo |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| matokeo ya utafutaji yanayokufaa zaidi, yanayolingana na utafutaji wako wa awali na shughuli kutoka kwenye huduma nyingine za Google.<br><br>**Kulingana na mipangilio yako, ili kukuonyesha matangazo yaliyowekewa mapendeleo kutokana na mambo yanayokuvutia.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Ukitafuta "baiskeli za kukwea milima" au utazame video za kukwea milima kwa baiskeli, unaweza kuona tangazo la vifaa vya spoti katika matokeo yako ya utafutaji au kwenye YouTube.<br>• Ukitazama video kuhusu kuoka kwenye YouTube, unaweza kuona matangazo zaidi yanayohusiana na uokaji unapovinjari kwenye wavuti.<br>• Pia unaweza kuona matangazo yanayokufaa kulingana na | a na Akaunti yako ya Google, mara unazotazama na kutumia maudhui na matangazo na shughuli zako kwenye tovuti na programu za wengine zinazotumia huduma zetu. Unaweza kukagua na kudhibiti data ya shughuli inayohifadhiwa kwenye Akaunti yako ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana | yanayokuvutia, kama vile matangazo yanayohusiana na uokaji unapovinjari kwenye wavuti baada ya kutazama video kuhusu uokaji kwenye YouTube. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| maelezo kutoka kwa mtangazaji. Kwa mfano, ikiwa umenunua kwenye tovuti ya mtangazaji, anaweza kutumia maelezo ya kuingia kwenye tovuti yake kukuonyeshe matangazo. | kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| **Kupima utendaji - Tunatumia data kwa ajili ya takwimu na upimaji ili kufahamu jinsi huduma zetu hutumiwa.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Tunachanganua data kuhusu jinsi unavyotembelea tovuti zetu ili kufanya mambo kama vile kuboresha muundo wa bidhaa.<br>• Tunatumia data kuhusu matangazo unayotangamana nayo ili kuwasaidia watangazaji kufahamu utendaji wa kampeni zao za utangazaji.<br>• Tunatumia data kuhusu sehemu ambazo watumiaji hubofya zaidi kwenye Google Earth ili kufahamu vipengele ambavyo ni maarufu na kutambua hitilafu.<br>• Huduma ya Tafuta na Google hupima mara ambazo hoja fulani imetafutwa na jinsi watumiaji hukadiria ubora wa matokeo yao ya utafutaji, ili kufanya | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  ◦ Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi.<br>  ◦ Taarifa binafsi unazotupa unapofungua Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  ◦ **Kufahamu jinsi watu hutumia huduma zetu ili kuhakikisha na kuboresha utendaji wa huduma zetu.** Kwa mfano, kuchanganua matumizi ya Google Tafsiri ili kuboresha ubora wa tafsiri na kuongeza upatikanaji wa huduma ya Tafsiri katika lugha nyingi.<br>  ◦ **Kutambua, kuzuia au kushughulikia vinginevyo ulaghai, matumizi mabaya, usalama au hitilafu za kiufundi kwenye huduma zetu.** |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| huduma ya Tafuta iwafae zaidi.<br>• Huduma ya Google Tafsiri huchanganua data kuhusu idadi ya tafsiri zilizotolewa na mara ambazo tafsiri imewekewa alama kuashiria kuwa ni duni, ili kutambua vipengele vipya vinavyohitajika na kushughulikia matatizo ambayo watumiaji wanakumbana nayo kwenye huduma.<br>• Tunaweza kushiriki maelezo yasiyoweza kukutambulisha na washirika wetu kama vile watoa leseni za maudhui ili kuambatana na malipo ya mirabaha. | au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu:<br>  • Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za kuacha kufanya kazi na shughuli za mfumo).<br>  • Maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile hoja zako za | Kwa mfano, kufuatilia mitindo ya matumizi kwenye Google Earth ili kutambua hitilafu.<br>• **Kutoa, kudumisha na kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wetu.** Kwa mfano, kuchanganua mara ambazo tafsiri imewekewa alama kuashiria kuwa ni duni kwenye huduma ya Google Tafsiri ili kushughulikia matatizo ambayo watumiaji wanakumbana nayo kwenye huduma.<br>• **Kubuni bidhaa na vipengele vipya ambavyo ni muhimu kwa watumiaji wetu.** Kwa mfano, kuchanganua data kuhusu idadi ya tafsiri zilizofanywa kwenye huduma |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| | utafutaji, historia ya kuvinjari kwenye Chrome ambayo umesawazisha na Akaunti yako ya Google, mara unazotazama na kutumia maudhui na matangazo na shughuli zako kwenye tovuti na programu za wengine zinazotumia huduma zetu. Unaweza kukagua na kudhibiti data ya shughuli inayohifadhiwa kwenye Akaunti yako ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka | ya Google Tafsiri ili kutambua vipengele tunavyoweza kuzindua.<br>• **Kutimiza wajibu kwa washirika wetu kama vile wasanidi programu na wenye hakimiliki.** Kwa mfano, kutoa ripoti kwa watoa leseni za maudhui ili kuambatana na malipo ya mirabaha. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| | kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |
| **Kuwasiliana nawe - Tunatumia maelezo tunayokusanya, kama vile anwani yako ya barua pepe ili kuwasiliana nawe moja kwa moja.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br>• Tunaweza kukutumia arifa iwapo tutagundua shughuli za kutiliwa shaka, kama vile jaribio la kuingia katika Akaunti yako ya Google kutoka eneo lisilo la kawaida.<br>• Tunaweza kukujulisha kuhusu mabadiliko au maboresho yajayo kwenye huduma zetu.<br>• Ukiwasiliana na Google, tutahifadhi rekodi ya ombi lako ili kusaidia kutatua masuala yoyote ambayo huenda unakumbana nayo. | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  ◦ Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa zinazohusiana na bidhaa mahususi.<br>  ◦ Taarifa binafsi unazotupa unapofungua | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br>• Ili **kutekeleza mkataba** nawe, kama vile unapowasiliana na Google kwa ajili ya usaidizi au kujisajili ili kupata mawasiliano kuhusu masasisho ya bidhaa.<br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  ◦ **Kutoa, kudumisha na kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji ya watumiaji wetu.** Kwa mfano, kukufahamisha kuhusu huduma zetu, kama vile kukujulisha kuhusu |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| • Huduma za Google kama vile programu ya Picha, zinaweza kukutumia mawasiliano ya utangazaji kuhusu matoleo yake ya bidhaa kama vile matangazo ya uchapishaji, kulingana na mipangilio yako.<br>• Huduma za Google kama vile YouTube Premium na YouTube Music Premium zinaweza kukuarifu kuhusu mabadiliko yajayo kwenye usajili wako. | Akaunti ya Google (kama vile jina na nenosiri lako, nambari ya simu, tarehe ya kuzaliwa au maelezo ya malipo).<br>• Taarifa tunazokusanya unapotumia huduma zetu:<br>  • Maelezo kuhusu programu, vivinjari na vifaa vyako, kama vile vitambulishi mahususi vinavyohusia na na kivinjari, programu au kifaa unachotumia; na maelezo kuhusu jinsi unavyotumia programu, vivinjari na vifaa na huduma zetu, (kama vile anwani za IP, ripoti za kuacha kufanya kazi na shughuli za mfumo). | mabadiliko au maboresho yajayo kwenye huduma zetu.<br>• **Kutangaza bidhaa ili kuwajulisha watumiaji kuhusu huduma zetu.** Kwa mfano, kuwatumia barua pepe watumiaji wa programu ya Picha kuhusu ofa ya uchapishaji. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | • Maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, kama vile hoja zako za utafutaji, historia ya kuvinjari kwenye Chrome ambayo umesawazisha na Akaunti yako ya Google, mara unazotazama na kutumia maudhui na matangazo na shughuli zako kwenye tovuti na programu za wengine zinazotumia huduma zetu. Unaweza kukagua na kudhibiti data ya shughuli inayohifadhiwa kwenye Akaunti yako ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| | inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za | |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| | saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |
| **Kulinda Google, watumiaji wetu na umma**<br><br>**Ili kusaidia kuboresha usalama na uaminifu wa huduma zetu, ikiwa ni pamoja na kutambua, kuzuia na kushughulikia ulaghai, matumizi mabaya, hatari za usalama na matatizo ya kiufundi ambayo yanaweza kuathiri Google, watumiaji wetu au umma.**<br><br>Mifano ya shughuli za uchakataji:<br><br>• Tunakusanya na kuchanganua anwani za IP na data ya vidakuzi ili kulinda dhidi ya matumizi mabaya ya kiotomatiki. Matumizi haya mabaya | Taarifa zitakazochakatwa zitategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini zinaweza kujumuisha yafuatayo:<br><br>• Mambo unayobuni au kutupa:<br>  ◦ Maudhui unayobuni, kupakia au kupokea (kama vile picha, video, barua pepe, hati na malahajedwali). Dashibodi ya Google inakuruhusu udhibiti taarifa | Misingi ya kisheria ya kuchakata maelezo haya itategemea jinsi unavyotumia huduma za Google na mipangilio yako lakini inaweza kujumuisha yafuatayo:<br><br>• Panapohitajika **kwa sababu zetu halali** na za wengine, zikiwemo:<br>  ◦ **Kutekeleza madai ya kisheria, ikiwa ni pamoja na kuchunguza uwezekano wa ukiukaji wa Sheria na Masharti yanayotumika.** Kwa mfano, kuchanganua maudhui ili yatusaidie kutambua |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
| --- | --- | --- |
| sheria hukagua kila ombi, bila kubagua aina na mara nyingi sisi hukataa ombi linaloonekana kuwa pana sana au lisilofuatilia mchakato sahihi.<br>• Wakati mwingine wajibu wa kisheria hutuhitaji tuhifadhi maelezo fulani kwa madhumuni kama vile kuhifadhi rekodi za kifedha, maelezo kama vile malipo ambayo umefanya kwenye Google kwa ajili ya kodi au madhumuni ya uhasibu.<br>• Sheria na kanuni mbalimbali zinatuhitaji tuweke hatua za kuthibitisha kuwa watumiaji wetu wana umri unaofaa kutumia huduma zetu. Ili kusaidia kubaini umri wako, tunachakata tarehe ya kuzaliwa unayoweka. Tunachakata pia maelezo kuhusu shughuli zako katika huduma zetu, wakati umeingia au kuondoka katika Akaunti ya Google na tunatumia teknolojia ya mashine kujifunza | ya Google katika sehemu ya Shughuli Zangu.<br>• Taarifa za mahali, jinsi inavyoweza kubainishwa na GPS, anwani ya IP na data nyingine kutoka kwenye vitambuzi vilivyo kwenye kifaa chako au karibu nacho, kulingana kwa kiasi na mipangilio ya kifaa na ya akaunti yako.<br>• Maelezo kutoka kwenye vyanzo vinavyoweza kufikiwa hadharani, kama vile maelezo yanayopatikana hadharani kwenye mtandao (kama vile iwapo jina lako linaonekana katika makala ya gazeti la eneo lako) au kutoka kwenye vyanzo | • Wakati tuna **wajibu wa kisheria** wa kufanya hivyo, kama vile kuhifadhi maelezo fulani kwa madhumuni kama vile kuhifadhi rekodi za kifedha, au kuchakata na kuhifadhi maelezo ili kusaidia kuhakikisha kuwa watumiaji wana umri wa kutosha kutumia huduma zetu. |

| Jinsi tunavyochakata data na sababu ya kuchakata | Aina ya data inayochakatwa | Misingi ya kisheria |
|---|---|---|
| ili kubaini kama unaweza kuwa umepitisha umri wa miaka 18. Katika hali fulani, iwapo hatuwezi kuthibitisha kuwa una umri wa kutosha kutumia huduma zetu kupitia njia nyingine, tunaweza kuomba maelezo mengine ili kuthibitisha umri wako, kama vile kitambulisho chako cha serikali, kadi ya mikopo, picha yako, au nambari yako ya simu. | vingine vya umma.<br>• Maelezo kutoka kwa washirika wetu tunaowaamini, kama vile kutoka kwa huduma za saraka, ambao hutupa maelezo ya biashara yatakayoonyeshwa kwenye huduma za Google, au washirika wa usalama wanaotupa maelezo ya kulinda dhidi ya matumizi mabaya. | |

## Kuunganisha huduma zako za Google

Ikiwa wewe ni mtumiaji unayeishi katika Umoja wa Ulaya, tunakupa chaguo la kuendelea kuunganisha huduma fulani za Google. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu huduma zako ulizounganisha na jinsi ya kudhibiti chaguo zako katika sehemu ya Kuhusu DMA na Huduma Zako Zilizounganishwa.

KUHUSU SERA HII

